
# FASIHI, LUGHA NA UTAMADUNI WA KISWAHILI NA KIAFRIKA

*Kwa Heshima ya Prof. M.M. Mulokozi*



**Wahariri**

**SHANI OMARI na METHOD SAMWEL**

Ni shahiri na jahara kuwa historia ya fasihi na taaluma za Kiswahli haiwezi kuelezwa bila jina la M.M. Mulokozi kutajwa. Kwa hiyo, inatia moyo sana kuona kitabu hiki cha kumuenzi Profesa huyu; hasa kwa vile aghalabu jadi ya kuwaenzi mashujaa wetu, wawe wa kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii kwa jumla, imekuwa ikihifadhiwa kwa ajili ya waliotutoka tu.

Inatia moyo zaidi kuona kuwa wengi wa wachangiaji katika kitabu hiki ni vijana ambao wameamua kushadidia jadi hii ya kuwaenzi watu waliotoa mchango mkubwa katika maendeleo ya lugha hii kuu ya Afrika na fasihi yake. Ari ya kuona upya fulani katika nyanja mbalimbali za lugha na fasihi ya Kiswahili inajitokeza katika kitabu hiki, hasa kuhusu suala la nadharia. Mathalani, kuhusishwa kwa **Ujumi wa Mtu mweusi** na pia **Ubuntu** kama ilivyofanyika katika Sura ya Tatu ya kitabu hiki ni dalili tosha kuwa vijana wameanza kusaili, kuchokonoa, kulabizi, na kuuliza maswali kuhusu uhalali na ustahiki wa kutumia nadharia ngeni na za nje ya Afrika katika kufanyia tafiti na kuchambulia matokeo ya tafiti hizo za masuala ya Afrika.

Kitabu hiki ni hazina kuu ambayo haitamfanya msomaji amwelewe tu gwiji huyu vizuri zaidi, bali pia ni buku litakalochochea mijadala ya masuala mbalimbali ya fasihi, lugha na utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika katika ngazi mbalimbali shuleni, vyuoni, na kwa wasomaji na watafiti wa kawaida.

*F.E.M.K. Senkoro, Profesa wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Namibia, Windhoek, Namibia.*

.....

Chapisho hili la kipekee ni mchango maridhawa wa makala za kitaaluma zinazopiga muhuri baraste za kiusomi alizopitia muadhama, mtaalamu na msomi wa Kiswahili, Mugyabuso Mulokozi. Ni makala zinazocheua fikra pevu za wataalamu waliobobea katika tasnia mbalimbali za bahari kuu ya Kiswahili. Ama kwa hakika, zao hili la kitaaluma bila shaka litamlimbua sio tu limbukeni wa taaluma hii bali pia kumjuza mengi mpenzi shadidi wa Kiswahili.

*Clara Momanyi, Profesa wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Afrika Mashariki, Kenya.*

**ISBN: 978 9976 5316 1 9**

**Kimepigwa Chapa na TUKI**
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

YALIYOMO UKURASA


Taarifa za Waandishi..... vii
Shukurani..... xvi
Tahariri..... xvii
Dibaji xi
Kulikoyela K. Kahigi.....

**Sehemu ya Kwanza: Wasifu wa Mulokozi** 1

1 Profesa Mugyabuso Mlinzi Mulokozi: Upekee wake Kitaaluma na Kijamii
*Edith Lyimo*..... 2

**Sehemu ya Pili: Mchango wa Mulokozi Kitanzu** 41

2 Mchango wa Mugyabuso Mlinzi Mulokozi katika Maendeleo ya Fasihi ya Watoto nchini Tanzania
*Leonard H. Bakize*..... 42

3 Mchango wa M.M. Mulokozi katika Ukuzaji na Uendelezaji wa Ushairi wa Kiswahili
*Pendo Mwashota*..... 61

**Sehemu ya Tatu: Falsafa na Nadharia** 81

4 Ujumi wa Mtu Mweusi katika Kazi za Nathari za M.M. Mulokozi
*Shani Omari*..... 83

5 Ujumi wa Mtu Mweusi katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka Washairi Teule
*Tumaini J. Sanga*..... 111

6 Usimulizi katika *Nagona* na *Mzingile*: Aina

na Athari zake kwa Msomaji
*Rose Jackson Mbijima*..... 132

7 Mbinu za Kisanaa Zinazosawiri Falsafa ya Ubuntu katika Tamthilia ya *Tambueni Haki Zetu*
*Anna Nicholaus Kyamba*..... 159

8 Mikondo ya Mtiririko wa Kishairi: Mabadiliko ya Ushairi wa Kiswahili wa Kezilahabi na Mulokozi
*Roberto Gaudioso*..... 180

9 Mwingilianomatini katika Riwaya za Shaaban Robert: Mifano kutoka *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1967)
*Felix Kwame Sosoo*..... 207

10 Mtagusano wa Kiusemezano kati ya *Utenzi wa Mwana Kupona*, *Utenzi wa Fumo Liyongo* na Riwaya za *Siri Sirini*
*Ombito Elizabeth Khalili*..... 230

11 Uhusiano wa Itikadi na Mtazamo wa Mtunzi: Uchunguzi wa Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed
*Murithi Joseph Jessee, Richard Makhanu Wafula* na *Kitula Geofrey King'ei*..... 253

**Sehemu ya Nne: Fasihi na Utamaduni**

12 Mulokozi na Suala la Ujadi Kupitia Mazigazi ya Mianzi
*Athumani S. Ponera* ..... 278

13 Utambulisho wa Mswahili: Mjadala Endelevu Uletao Changamoto ya Kuifasili Fasihi ya Kiswahili na Utamaduni wa Mswahili
*Wallace Mlaga* ..... 293

14 Dhana ya Maadili katika Uandishi wa Shaaban Robert na Nafasi yake katika Muktadha wa sasa nchini Tanzania
*Aldin K. Mutembei* ..... 320

15 Matumizi ya *Istilahi-Jadi* katika Fasihi na Jamii Kupitia Tendi za Kiswahili: Mifano kutoka *Utendi wa Rukiza*
*Neema B. Sway* ..... 352

16 Ushairi wa Kiswahili kama Chombo cha Utetezi wa Mwanamke: Mwangwi wa Jana au Uhalisi wa Leo?
*Clara Momanyi* na *Joseph Maitaria* ..... 375

**Sehemu ya Tano: Uandishi na Uchapishaji** 403

17 Dhana Kanganyifu katika Uchapishaji na Uchapaji kama Msingi wa Kuielewa Tasnia hiyo
*Timothy T. Mapunda* ..... 404

18 Makosa ya Kiuhariri katika Vitabu vya Kiada vya Kiswahili nchini Tanzania
*Festo N. Joster*..... 419

19 Matatizo ya Uandishi katika Kiswahili: Maana, Chanzo na Ufumbuzi
*Titus Mpemba*..... 442

**Sehemu ya Sita: Maendeleo ya Lugha Kisera na Kiistilahi** 475

20 Mchango wa Viongozi wa Kenya katika Kuimarisha Lugha ya Kiswahili
*Pamela M.Y. Ngugi*..... 476

21 Mikakati Inayotumiwa na Vyombo vya Habari nchini Kenya Kukabiliana na Changamoto za Kiistilahi
*Stanley Adika Kevogo, Mwenda Mukuthuria* na *James Omari Ontieri*..... 497

22 Ulinganishi wa Kimsamiati Baina ya Kiswahili Sanifu na Kimakunduchi
*Mussa M. Hans*..... 531

23 Michakato Mipya ya Kueneza Dini Kiutandawazi na Athari zake katika Mustakabali wa Kuenea kwa Kiswahili
*Alex Umbima Kevogo, Mwenda Mukuthuria* na *Ayub Mukhwana* ..... 549

**Sehemu ya Saba: Fasihi na Tafsiri** 577

24 Uzingativu wa Vipengele vya Kifani katika Kazi za Fasihi ya Kiswahili Zilizotafsiriwa: Mifano kutoka Tamthilia ya *Julius Caezar*
*Edson Z. Thomas*..... 578

25 Tafsiri katika Fasihi ya Ulimwengu: Mchango, Changamoto na Mapendekezo
*Hadija Jilala*..... 607

# 22
# Ulinganishi wa Kimsamiati Baina ya Kiswahili Sanifu na Kimakunduchi

Mussa M. Hans

## 1. Utangulizi

Kumekuwa na mjadala endelevu kuhusu lahaja za Kiswahili hususan idadi yake, namna zilivyoinukia na uhusiano wake na Kiswahili sanifu. Matokeo ya mjadala huo ni wataalamu kutofautiana kuhusu idadi ya lahaja za Kiswahili, majina ya lahaja hizo, namna zilivyoinukia na uhusiano wake na Kiswahili sanifu. Mathalani, kuna baadhi ya wanaisimu kama Massamba (2007) wanaamini kwamba hizi tunazoziona hivi leo kama lahaja za Kiswahili zilianza kama lugha kamili za Kibantu na kwamba lahaja hizi ziliinukia sawia katika maeneo mbalimbali ya upwa wa Afrika Mashariki. Wataalamu wengine kama Nurse na Spear (1985) wanaamini kwamba lahaja hizi ziliinukia sehemu moja na baadaye kutawanyika katika maeneo mbalimbali ya upwa wa Afrika Mashariki. Kuna wataalamu wengine pia, wanaeleza kwamba baadhi ya lahaja kama Kimakunduchi zinafanana zaidi na lugha nyingine za Kibantu kuliko zinavyofanana na Kiswahili sanifu (taz. k.m. Massamba, 2007).